JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

***Dar es Salaam, 29 Agosti, 2023***

# TAARIFA KWA UMMA

## MWENENDO WA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

### 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Pili ya Udahili na zoezi la kuthibitisha udahili kwa waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Kwanza ya Udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2023/2024 litakamilika **Jumatano tarehe 6 Septemba, 2023**. Zoezi litakaloendelea ni vyuo kuchakata na kuidhinisha maombi ya udahili yaliyopokelewa vyuoni katika Awamu ya Pili ya Udahili. Zoezi la kuchakata na kuidhinisha maombi hayo litakapokamilika, majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Pili ya Udahili yatatangazwa na vyuo husika tarehe **20 Septemba, 2023.**

Baada ya kukamilika kwa Awamu ya Pili ya Udahili, Awamu ya Tatu ya Udahili wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2023/2024 itaanza rasmi tarehe **25 hadi 29 Septemba, 2023*.*** Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao bado hawajatuma maombi ya udahili mpaka sasa watumie muda huu uliobaki vizuri kutuma kwa usahihi maombi yao ya udahili kwenye vyuo wanavyovipenda.

Tume inaelekeza Taasisi za Elimu ya Juu nchini kuendelea kutangaza programu ambazo bado zina nafasi. Aidha, waombaji na vyuo wanahimizwa kuzingatia utaratibu wa udahili kama inavyoonekana kwenye kalenda ya udahili iliyoko katika tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

### 2.0 MWENENDO WA UDAHILI

Zoezi la udahili wa Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini linaendelea vizuri. Waombaji wanaendelea kutuma maombi yao katika Awamu ya Pili ya Udahili. Wale waliopata udahili katika chuo zaidi ya kimoja wanaendelea kujithibitisha kwa kutumia namba za siri walizotumiwa kwa njia ya ujumbe mfupi au Barua pepe.



Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

Mpaka sasa jumla ya waombaji **23,387** waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja, kati ya **43,213** wameshajithibitisha katika chuo kimojawapo. Hivyo, Tume inawahimiza wale ambao bado hawajajithibitisha wakamilishe uthibitisho wao kwa kupitia akaunti zao kwenye vyuo wanavyovipenda. Hakuna mwanafunzi atakayekosa chuo kwa kushindwa kujithibitisha.

Katika zoezi la udahili linaloendelea, Tume inasisitiza yafuatayo kwa Vyuo vya Eimu ya Juu na waombaji udahili:

a) Waombaji wanasisitizwa wasome miongozo ya sifa ya kujiunga na programu husika ili kuona kama wanakidhi vigezo kabla ya kutuma maombi ya udahili. Miongozo hii "*Admission Guidebook"* inapatikana katika tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz). *Pia vyuo husika vimeweka vigezo mahususi katika kila programu.*

b) Waombaji wenye changamoto ya kupokea namba ya siri ya kujithibitisha katika chuo kimojawapo, wanaelekezwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

c) Kwa urahisi wa kupokea namba za siri za kujithibitisha, waombaji wanashauriwa kutumia Barua pepe zao au mitandao ya simu ya TTCL, TIGO, Airtel, Vodacom na Zantel.

d) Uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili.

e) Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini zinazofanya udahili wa Shahada ya Kwanza zihakikishe zinaruhusu waombaji udahili kuingia katika mifumo yao na kuwapa *"password*" na "*username"* ili wafanye udahili na kujithibitisha wao wenyewe.

f) Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini zihakikishe waombaji udahili wanajithibitisha wao wenyewe kupitia akaunti zao na si vinginevyo.

g) Waombaji wanaotaka kubadili uthibitisho wao, waingie katika akaunti za vyuo walivyojithibitisha na kufuta uthibitisho wao wa awali ili wajithibitishe katika chuo kingine wanachokipenda.

h) Waombaji wanaotaka kubadili maombi yao ya udahili waingie katika akaunti zao za vyuo walivyodahiliwa na kufuta udahili wao ili kutuma upya maombi yao.

i) Vyuo vya Elimu ya Juu vinasisitizwa kuendelea kuelimisha umma namna sahihi ya kuwasiliana na vyuo husika ili kuepuka udangayifu unaoweza kujitokeza.



Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

Aidha, Tume inapenda kufahamisha umma kuwa waombaji udahili wote wanaoshiriki mafunzo kwa mujibu wa sheria katika Kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kutokuwa na hofu kwani wote watapata fursa ya kujithibitisha kabla ya mwaka wa masomo kuanza.

## 3.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI NA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha au kutaka kubadilisha uthibitisho wao, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozona taratibu zilizowekwa. Hivyo, wawasiliane na vyuo wanavyotaka kujithibitishakupitia madawati yao na vyuo vitapokea taarifa zao na kuzifanyia kazi.

Tume inaelekeza Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini zinazofanya udahili wa Shahada ya Kwanza kuendelea kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika zoezi la udahili ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima kwa waombaji udahili na wananchi kwa ujumla.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa
**KATIBU MTENDAJI**
**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA**



Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz